

ALIISHI MIONGONI MWETU

Picha za kupendeza
pamoja na
mazungumzo




kitagusa moyo wako
na kinaweza kubadili
hatima yako ya milele



Zaidi ya nakala **milioni 18**
zimechapwa katika lugha 27





Katika mwaka wa 30 B.K, Himaya ya Kirumi ilikuwa imetimiza miaka 780. Ilijumuisha nchi zote zilizozunguka Bahari ya kati, kutoka Hispania na Galatia mpaka Misri na Siria.



...Yaliyopiga kambi Yerusalemu, ambao ulikuwa mji mkuu wa Yudea katika Palestina na ambao ulikuwa sehemu ya Jimbo la Siria.

Siku moja katika Ikulu ya Gavana wa Kirumi, Pilato aliyekuwa kiongozi wa majeshi ya uvamizi.



Kapteni, je una habari gani kuhusu matukio ya juma hili?

Gavana nimeona umati mkubwa wa watu karibu na mto Yordani ambapo mtu mmoja aitwaye Yohana Mbatizaji amekuwa akihubiri anaaminiwa kuwa ni nabii.



Anabatiza watu na kungumza juu ya kuja kwa kiongozi mpya anayeitwa Masiha.

Mm... nahisi ni kiongozi mpya, ambaye atakusanya jeshi na kujaribu kutuondoa sisi Warumi kutoka hapa...



Siye wa kwanza na wala hatakuwa kiongozi wa mwisho, lakini hakuna hata mmoja ambaye mpaka sasa ameishafanikiwa kutuondoa sisi hapa.

Ndiyo, hawa Wayahudi kwa hakika ni watu wa kipekee.



Ndiyo watu pekee ambao hawawezi kuvunjwa vunjwa.... na mfalme Tiberia anakubaliana na mwenendo wao. Wakati nilipokuwa nimepamba Ikulu hii na picha za dhahabu, kuonyesha miungu yetu ya kirumi, yeye aliniamuru niziondoe.

Kwa Wayahudi ilikuwa ni kunajisi mji wao mtakatifu. Ni marufuku kabisa kuonyesha picha yoyote ya Mungu wao. Ishara zetu zote, ambazo zinahusiana na ufalme wetu wa Kirumi wanaziona



kama kufuru. Hivyo walipeleka malalamiko kwa mfalme Tiberia..... na wakashinda kesi.

Ni watu wa gumu sana kuwatawala. Kazi yanguhapa Yerusalemu kama Gavana ni mbaya zaidi kuliko popote katika Himaya nzima!



Hiyo ni kweli kabisa hawa Wayahudi ndio pekee katika Himaya yote ambao hawajisikii kuabudu miugu yetu ya Kirumi.



Hawalazimiki kufanya kazi siku ya sabato na pia wana hiari kumkatalia mtu yeyote yule asiye Myahudi kuingia katika hekalu lao eti kwa kuwa wao tu ndio Taifa teule.



Oh! hili hekalu la Yerusalemu! ni hali ya kutisha wakati mahujaji 200,000 wanapowasili kwa sherehe za Kiyahudi, mtu lazima awe mwangalifu sana kabla hajaelewa kumetokea nini. Wataanza ghasia na kuleta machafuko.



Tunafuatilia sana mwenendo wao kutoka kambi yetu ya Antonia na tunawaza kuzuia ghasia yoyote mapema.



Haya Kapteni, fuatilia kwa makini matukio hayo ya mto Yordani na uendelee kunipasha habari....



Ninaenda pale mimi mwenyewe, nawafahamu viongozi wa Kiyahudi wa pale. Nao pia wanashangazwa na mtu huyu Yohana Mbatizaji. Wana mpango wa kumfanyia uchunguzi wao....

Siku iliyofuata kwenye mto Yordani.



Huyu nabii kutoka jangwani hakika anavutia watu wengi... hebu tuone ni kwa sababu gani.

Sikilizeni ninyi nyote, kuna habari njema! yule Masiha ambaye ni KRISTO amekuja! Atajitambulisha hivi karibuni na ataonekana hadharani.



Siku ya hukumu inakuja pamoja naye. Panga lake la kuvunia liko mkononi tayari kukusanya ngano na kuweka ghalani.



Lakini atachoma makapi kwa moto usiozimika! Tayarisheni mapito, ondoeni viziwi vyote, tengenezeni njia iliyonyooka kwa ajili yake.



Nini? eti Masiha amekuja? Basi atawaondoa Warumi! Ukombozi umefika, miaka ya neema itanza hivi karibuni!


Hatujaipata mtu wa Mungu kama Yohana Mbatizaji kwa muda mrefu.

Anaishi maisha magumu kama yale ya mitume wa zamani.... Anavaa mavazi yaliyotengenezwa na nywele za

ngamia, ana mkanda wa ngozi kiunoni mwake. Anakula nzige waliobanikwa na asali ya porini.




Kama nimemuelewa sawa sawa, kila mtu anapaswa kubadilika moyo wake na kumtumikia Mungu, siyo nafsi yake mwenyewe.





Wakati huo mtu mmoja aitwaye Yesu wa Nazareti anatoka kwenye umati...

Na anasonga mbele kumwelekea Yohana Mbatizaji na kusema;







Yesu alibatizwa kwenye mto Yordani akiwa na miaka 30. Yeye alikuwa nani? Aliitwa mwana wa Yusufu, Seremala wa Nazareti, jina la mama yake alitwa Mariamu, ndugu wa mama wa Yohana mbatizaji. Wazazi wake wangeeleza habari za kuisimua juu ya mambo ya kiungu yaliyoambatana na kuzaliwa kwake.



Unajua habari ya nabii Danieli? Malaika Gabrieli alimuelezea habari za kuzaliwa kwa Masiha. Sijui kama tutaiona siku hiyo ya ajabu.

Ninaamini tutaiona kwa sababu...



Siku moja ya sabato, wazazi wa Mariamu walirudi nyumbani kutoka hekaluni.

Kulingana na unabii wa Danieli mambo haya yanapaswa kutimia nyakati hizi.

Mariamu, nenda ukalete taa ya mafuta na kuandaa chakula tafadhali....



Ghaffa... Furahi Mariamu! Umepata upendeleo mkubwa kutoka kwa Mungu!



Kuna nini? Hizi salamu ni za nini? Je inawezekana kuwa ni ujumbe kutoka mbinguni?

Usiogope Mariamu utapata mimba na utazaa mtoto wa kiume nawe utamwita 'Yesu' yeye ndiye Masiha.





Mbona sielewi. Nitawezaje kupata mtoto nami ningali Bikira?



Mimi ni mtumishi wa Bwana ifanyike kama ulivyosema.

Roho Mtakatifu atakuja juu yako na nguvu za aliye juu zitakufunika hivyo yule mtakatifu atakayezaliwa ataitwa mwana wa Mungu. Ili kukuhakikishia kwamba yale nayokwambia yatatokea, binamu yako Elisabeti naye atapata mtoto katika siku za uzeeni. Yeye anayesemwa kuwa ni tasa, sasa ana mimba ya miezi sita. Kwa sababu hakuna lisilowezekana kwa Mungu!

Siku chache baadaye...



Mama, ningependa kwenda kukaa na binamu Elisabeti kwa majuma machache.

Naona unataka sana kufanya hivyo na moyo wako wote ingawa hutaki kusema kwa nini.....



Kuwatembelea kwako, kwa kakika kutafanya awe na furaha yeye na mume wake Zakaria. Lakini wanakaa mbali sana kutoka hapa, ni kule Yudea.

Utaweza tu kwenda kama utajiunga na msafara unaopita hapa Nazareti ukielekea Yerusalemu.

Punde Mariamu anaanza safari yake kuelekea Yudea.



Lakini nitakukabidhi kwa kiongozi mwaminifu atakayekutunza.

Mimi siopopi kwa sababu najua Munga atanilinda.



Mungu amenibariki na uwepo wake na amezungumza na moyo wangu ya kwamba nitakuwa mama wa Masiha atayetuokoa na dhambi zetu... sasa nina shauku kuhusu hali ya binamu yangu, na pia kujua kuwa yote ni kweli.



Mariamu wa Nazareti, hiyo ndiyo njia ya Ain-karin, ambapo binamu yako Elisabeti anaishi. Kijiji kipo kwenye bonde lile.

Asante kwa kunisindikiza na Mungu azidi kukulinda.

Mariam alipowasili



Binamu Elisabeti, amani na furaha ya Mungu i juu yako!

Mariam kutoka Nazareti, hii ni ya kushangaza!



Kunafanyika nini ndani yangu? Ghaffa mtoto ninayembeba anaanza kurukaruka ndani yangu!



Marimu, Ugeni huu una maanu gani?

Oh, Elisabeti ni furaha gani kukuona mjamzito

...hii inamaanisha ya kuwa yote yaliyosemwa kwangu yametoka kwa Mungu na yatakuwa kweli.

hata bila kutarajia

Kwanza, ningependa kukueleza siri yangu...

Mariam, ni vema sana umeamini meneno ambayo Mungu amekuambia

Ninakiri kwako...



Niliposikia sauti yako mtoto wangu aliruka tumboni. Hiyo ni ishara! Kwa nini

nimependelewa kiasi hicho, hata mama wa Masiha aje kwangu?





Umebarikiwa wewe kati ya wanawake wote na amebarikiwa mtoto unayembeba!



Nafsi yangu inamtukuza Bwana! Ameangalia unyonge wa hali yangu, yeye aliye mkuu amefanya mambo makubwa ili jina lake lizidi kutukuzwa.

Zakaria huyo anakuja, hawezi tena kuzungumza

Nitakueleza yote baadaye



Mariamu, Zakaria amekuwa bubu, imetokana na mimba yangu...

Na pia inahusu mimba yako



Unajua hatukuwa na watoto na hatukuwa na tumaini lolote la kuwapata



Miezi sita iliyopita, Zakaria alienda Hekaluni mwa Bwana na makuhani 300 wa kundi lake, kumtumikia Bwana, Mungu wetu...



Pigeni kura kuchagua jina la Kuhani atakayekuwa na heshima ya kutumika kwenye hekalu la Bwana na kuchoma uvumba.

Ni kuhani Zakaria!

Ni nafasi ya kipekee katika maisha yangu! Nitaingia katika uwepo wa Bwana.







Hatimaye Zakaria anatoka!

Anaonekana hana furaha, kwa nini anatumfanyia ishara kama vile

ghafila hawezi tena kunena..

...Ni lazima ameona maono..

..Ama amepokea ufunuo.



Na sasa nina mimba ya miezi sita

Mungu wetu ni mkuu sana. Ameniondolea aibu yangu..

Mariamu alikaa miezi mitatu na Elisabeti na baadaye alirudi nyumbani Nazareti. Siku ilifika ambapo Elisabeti alijifungua mtoto wa kiume. Na siku ya nane walikuja kumtahiri mtoto. Na wakati huo mtoto alipewa jina.

Basi, kutahiri kumekamilika.



Jina gani ambalo mtampa mtoto huyu?

Ataitwa Yohana



Ni jina zuri! maana yake Mungu ni mwenye huruma'

Lakini hakuna mtu kwenye ukoo wenu mwenye jina hilo!



Zakaria kwa vile wewe ndiye baba yake, unamuji wako ni wa nini?




Kinywa cha Zakaria kimefunguka na anaweza tena kunena!



Miezi kadhaa baada ya
Mariamu kurudi Nazareti...



Sina shaka!
Mariamu niliyemposa
ni mjamzito.
Inawezekana hakuwa
mwaminifu kwangu?
Ni lazima
nimulize.



Yusufu, ni lazima
uniamini! Nimepokea
ujumbe kutoka
mbinguni....

Hali yangu
ni kazi ya Mungu!
inabidi nimzae
Masiha!



Mariamu
nawezaje
kuamini
haya?...

6.Ni jambo
lisilowezekana!



...Lakini sipendi
ajulikane
hadharani na kuaibishwa.
Kwa hiyo nitaachana
naye kwa siri.



Kwa sababu mimi
si baba wa mtoto
huyu, nitamwacha
Mariamu....

Siku moja alipoamka asubuhi...

Ni ndoto ya ajabu!...

Sina shaka ni Mungu amezungumza nami kupitia malaika wake!

Najua Mariamu hasemi uwongo.

Naye atakuwa Masiha...

...Naye atatoka katika ukoo wa mfalme Daudi!

Kwa vile Mariamu na mimi tunatoka katika ukoo wa kifalme wa Daudi...

Huyu mtoto atatimiza unabii.

Sasa naelewa ni kitu gani Mungu anachotaka nifanye!

Basi nimefanya uamuzi. Nitamchukua Mariamu kama mke wangu mara moja!

Muda mfupi baadaye, harusi ya Yusufu na Mariamu inasherehekewa.

Mariamu, mpendwa, karibu, kwenye nyumba hii kuanzia sasa na kuendelea ni ya kwako pia.



Miezi michache baadaye pale Nazareti.....



Kaisari Augusto ametoa amri ya kusajili majina ya watu wa Himaya yote ya Kirumi, kila kiongozi wa nyumba anatakiwa kwenda kwenye mji wake ili kujiandikisha.



Tena? ujanja mwingine wa Warumi ili kupandisha kodi

Au wanataka kujua idadi ya wananchi wenye uwezo wa kufariya maasi kupinga utawala wao.



Ukoo wa Daudi ambao ni asili yangu unatoka Bethlehemu

Muda si mrefu Mariamu atajifungua, hivyo nitachukua

Siku chache baadaye



Mwisho we! Bethlehemu!



Watu wengi sana! Yusufu tutapata wapi chumba?

kwa ndugu zangu hiyo ni hakika, lakini ngoja kwanza nitimize taratibu zote za kiofisi.

Kwenye ofisi ya usajili

Simameni kwenye mstari! Sikilizeni kwa makini! Maelezo ya uongo yatamletea mhusika adhabu kali

Yesse, nimekasirika sana! Kama mzaliwa wa ukoo wa mfalme Daudi ninalazimishwa kutoa mahesabu kwa hawa Warumi

Ninavyoamini mimi, utawala wao hautadumu kwa muda mrefu zaidi



Nyoto mpya imegunduliwa. Je takuwaje ikiwa inamaanisha kuwa Masiha anakuja?


"Kumbuka unabii wa Balaamu. Nyota itatoka Israeli naye atakuwa mtawala mkuu".

Kwenye nyumba ya ndugu...



Usiku ule Mariamu alijifungua mtoto wake wa kwanza wa kiume...

Alimfunika kwa nguo na kumlaza kwenye hori la ng'ombe.....



Kwenye makonde ya Bethlehemu kulikuwa na wachungaji wanaolinda mifugo usiku...



Habari njema kwenu nyote! Mtoto amezaliwa kwenu – mwokozi! Mtamkuta amelazwa katika hori la ng'ombe pale Bethlehemu

Hebu twende na tuone!

Amezaliwa usiku wa nyota mpya – kwenye zizi – na ni Bethlehemu mji wa kuzaliwa Daudi ukoo wote upo hapa!

Hii ni ishara! Atakuwa mchungaji wa baadaye wa watu wetu, Masiha aliyeahidiwa!



Mungu amekuja kwetu. Anga yote imejaa nuru, ninasikia nyimbo za utukufu kwa Mungu aliye juu!

Hakika huyu ndiye mtoto aliychaguliwa



Siku ya nane mtoto alitahiriwa. Tohara ilifanywa kwa watoto wote wa kiume wa Kiyahudi kama ishara na nembo ya ahadi ya Mungu kwa Ibrahimu.

Siku iliyofuata habari ilienea haraka.



Yusufu jina gani unampatia mtoto huyu?

Jina lake ni Yesu!

Maana yake ni Mungu ametuokoa!

Wazazi wa Yesu walikuwa na kumbukumbu nyingi za silku za ujana wake! Moja wapo ni siku ya arobaini baada ya kuzaliwa.



Mariam, kulingana na sheria ya Mungu, kila mzaliwa wa kwanza wa kiume ni lazima awasilishe mbele za Bwana



Hekalu la Yerusalemu haliko mbali kutoka hapa. Hebu twende na tumpeleke mtoto kwa Mungu!

Oh, Yusufu mtafurahia sana hatua hiyo

Nje ya Hekalu....



Kondoo huyu ndiye anayefaa kwa dhabihu kamilifu

Hapana, ni ghali mno kwetu. Nitachukua hawa njiwa wawili.

Wakati huo mzee mmoja anaingia hekaluni, jina lake ni Simeoni, anajulikana sana na wengi.



Simeoni ni kitu gani kimekuleta hekaluni leo?

Anna, ninahisi nitakutana na mtu leo! Roho Mtakatifu amenituma

Simeoni anasema mara nyingi hatakufa kabla ya kumwona Masiha

Ni mzee gani yule pale?



Simeoni... mwangalie huyu mtoto!

Oh! Ni furaha isiyu kikomo nafsini mwangu!

Sasa naweza kufa, maana, macho yangu yameuona wokovu wa Bwana. Nuru yake itaangaza mataifa yote ta ulimwengu!





Nambariki mtoto huyu ambaye...

Atasababisha kuanguka na kuinuka kwa watu wengi duniani pote!

Wazazi wa Yesu pia walikumbuka tukio la wachunguza nyota. Kukutana kule kulionyesha vile Yesu alivyokaribishwa na wageni lakini alikataliwa na watu wake. Wakati wa kuzaliwa kwa Yesu, walwasili Yerusalem mamajusi (wenye hekima) kutoka mashariki.....



Yuko wapi mtoto aliyezaliwa, ambaye atakuwa mfalme wa Taifa hili?

Tumeiona nyota yake ikionekana kwenye nchi zetu.

Nini? Masiha amekuja?

Haiwezekani! tungejua Yerusalem! Lakini hakuna mtu aliyesikia chochote.

Mfalme anapaswa kusikia habari hizi mara moja!



Mtukugu!
kuna wageni
wanaomtafuta mtoto
ambaye ni Masiha
mtarajiwa!

Wanasema kuzaliwa kwake
kumeonekana kupitia
mpangilio wa nyota!

Nini? mtoto
atakuwa Masiha nami
sijapewa taarifa? kwa siri
mpinzani wa kiti changu
anainuliwa.



Inabidi
niwe mjanja ili
niweze kuifichua
hila hii!

Waite
Mafarisayo
mara moja!



Nimesikia tetesi kuhusu
kuwasili lwa Masiha. Inabidi
njiandae kwa hilo.
Mnafahamu nini kuhusu
familia yake na
mahali
atakapozaliwa?



Biblia takatifu inasema.
Masiha atakuwa wa
ukoo wa mfalme
Daudi

Na mfalme
Daudi anatoka
Bethlehemu.

Imeandikwa:
Bethlehemu, kutoka
kwako atakuja
mfalme ambaye
atakuwa mchungaji
wa watu
wangu.



Haraka, nenda
na walete mamajusi
wa kutoka
mashariki hapa!

muda mchache baadaye....

Nimefahamishwa kwamba
mnamtafuta mtoto
ambaye ni Masiha?

Ndiyo
tumeona
nyota yake!





Lini, kulingana na hesabu zenu alizaliwa?

ni wakati huu

Ninaweza kuwasaida: Amezaliwa Bethlehemu..... mtafuteni pale na mniletee mimi taarifa, ili na mimi pia niweze kwenda kumwabudu!



na punde wanampata mtoto



Dhahabu naileta kwa unyenyekevu kwa mzaliwa katika ukoo wa Daudi.

Ni atumaini yangu kwamba uvumba wenye kunukia utakuwa wa kupendeza kwa mjumbe wa Mungu.

Nallete manemane kwa ajili yake anayeelewa mateso yetu.

Wanaondoka Yersalemu na kuelekea Bethlehemu.....



Asubuhi iliyofuata, walipoamka...



Nilipata ndoto mbaya sana usiku uliopita... Nilimwona mfalme Herode akimkimbiza mtoto, akijanibu kumua.

Yusufu, chukua tahadhari! Hatumwamini mfalme Herode.

Mtoto huyu amemletea mashaka.

Hivyo, hatutarudi kwenye nchi zetu kupitia Yersalemu!



Wakati siku zinaendelea kupita.....Herode anangojea kwenye makao yake.



Baada ya kuwa ugenini kwa kitambo. Yusufu na Mariamu wanarudi Nazareti ya Galilaya. Pale Yesu alikua na kupata Hekima wakati akiwa mtii kwa wazazi wake. Akiwa na umri wa miaka thelathini alienda kwa Yohana Mbatizaji na akabatizwa.



Siku moja, Yohana Mbatizaji anamwona Yesu akipita...



Nawambia nyote wawili wafuasi wangu, mnamwona mtu yule?



Ndiye Mwanakondoo wa Mungu ambaye maandiko yanasema, Kama Mwanakondoo apelekwaye machinjoni, atachukua dhambi za ulimwengu juu yake.

Hii inamaanisha ya kwamba ndiye Masiha mhaidiwa, Kristo!



Ndiyo nilimwona Roho wa Mungu kutoka mbinguni akija juu yake... ndiyo maana nashuhudia ya kwamba ni mwana wa Mungu!

Njoo Andrea tumfuateli!



Mnatafuta nini?

Unaishi wapi? Tunataka kunena nawe...

Njoni muone.

Walikaa naye muda mrefu.....



Yale yalikuwa mazungumzo yenye kugusa moyo.

Inanipasa nimwambie kaka yangu Simoni sasa hivi!



Simoni! Simoni! tumempata Masiha! Kristo! harakisha nitakuongoza kwake!



Nini, Masiha? Kristo? Haiwezekani!



Wewe ni Simoni, mvuvi wa samaki, utaitwa Petro. Nifuate mimil!



Yesu, huyu ni Filippo. Ni rafiki yetu... pia anatoka Bethsaida...



Filippo nifuate na uwe mwanafunzi wangu.



Filippo aliondoka na akaenda kumweleza rafiki yake.





Yesu umekuja kwenye arusi, nimefurahi sana kukuona.



Lakini ningependa ujue hakuna divai iliyobaki! Je unaweza kutoa msaada wowote?



Mama, mbona unanihusisha mimi? Saa yangu haijawadia!

Birika langu ni tupu!



Najua, lakini nisikilizeni kwa makini.

Na hakuna divai iliyobaki

Yesu akiwaambia mfanye jambo fulani mfanye kama alivyowaelekeza!

pale kuna mabalasi sita ya kutawadhia, tafadhali yajazeni maji...



Kama utakavyosema Yesu



Yote yamejaa!





Sasa mpatieni mkuu wa meza anywe kwanza

Atacheka na kudhani tunamfanyia mzaha

Hapana sio hapa

Hebu jaribu hii....

Umepata wapi divai bora kama hii? Ni aina gani hii?

Kuna mabalasi sita ya divai hiyo!



mbona umetoa divai hafifu kwanza na umesaza divai bora mpaka wakati huu!

Hebu niambie wewe bwana arusi



Umefanya makosa! kwenye arusi divai bora hutolewa kwanza na baadaye ndipo divai hafifu hugawiwa



Mkuu wa meza hajui... Lakini tumemwona Yesu wa Nazareti kabadilisha yale maji kuwa divai

Ni muujiza, maji yamegeuzwa divai! Ni ajabu lakini ni kweli

Na karamu ya arusi yaweza kuendelea

Basi tufurahie tuwaimbie maarusi wimbo mwingine



Niamini, hakuna mwanadamu anaweza kutenda miujiza kama hii, ni Mungu peke yake, je inawezekana Yesu ndiye Masiha anayetarajiwa?



Divai ni mfano wa furaha ya maisha. Hii divai mpya bora inaashiria maisha mapya ya furaha yaliyoahidiwa na Mungu kwa njia ya Masiha.

Yesu alisafiri kwenda Kapernaumu karibu na ufuko wa ziwa la Genesareti, Yohana, Andrea na Petro walifanya kazi pale kama wavuvi.



Zile ndizo ngalawa zetu za kuvulia samaki. Ngalawa hii ni ya Simoni Petro



kaka yangu Yakobo na mimi tunajua shughuli zote za uvuvi



ninyi wavuvi mtakuwa wanafunzi wangu wa kwanza! nifuateni!



kila kitu kipo tayari kwa ajili ya uvuvi wa usiku



Yesu unaweza kulala nyumbani kwangu... mama mkwe wangu ni mgonjwa, yupo kitandani ana homa kali



haya twenda, Petro...niamini mimi, mama mkwe wako atapona!



najisikia nafuu! Ndio naona hali yangu ni nzuri sana nitainuka na kuwaandalia chakula



usiku ule Petro na wenzake walienda kuvua samaki

Asubuhi iliyofuata...



imekuwaje? Vikapu vyangu ni vitupu hakuna cha kuuza leo

tulikuwa na kazi ngumu sana usiku, lakini hatukupata kitu chochote! Inabidi sasa tunafishe nyavu zetu



4. Huyu aja Yesu akifuatwa na umati



Petro chukua ngalawa uipeleke nje kidogo ya ufukweni ili kwamba niweze kunena na watu wote hawa, ambao wanashauku ya kusikia neno la Mungu



mchana na usiku, awe amelala au yu macho mbegu ilichipuka na kukua

ingawa hajui ni kwa jinsi gani kwa uweza wake binafsi ardhi inatoa nafaka kwanza mche na baadaye kichwa na tena zao kamili ambalo kichwa chake kinatupa mkate wa kila siku



Yesu akasema hivi ndivyo ufalme wa Mungu unavyofanana, mtu alitawanya mbegu kwenye ardhi



Ninyi nyote mnakaribishwa kuingia! Lakini mnapaswa kubadilisha maisha yenu! Mioyo yenu haipaswi kuwa migumba kama mawe au kama udongo uliojaa miiba iliyokuwa na hamu ya vitu, fedha na starehe!...





Acheni kujidanganya nafsi zenu na wengine! Chunguzeni nia ya mioyo yenu! Muriгу anataka wakati wote mtende haki.

Pendeni kusamehe na tembeeni kwa unyenyekuvu na Mungu!



Yesu alipomaliza kufundisha alimgeukia Petro

Petro sasa nenda ukavue samaki... Peleka chombo chako kwenye kina kirefu na ushushe nyavu zako.

Mbona tumefanya kazi usiku mzima, na hatukupata kitu chochote.



Petro, nakuambia tena, peleka chombo chako na ushushe nyavu zako kubwa

Haitasaidia! Huu si wakati mzuri... samaki hawaelei tena juu ya maji!



Fanya kama nilivyokwambia, Petro! Niamini!

Ni kwa kuwa tu umeşa, ndio sababu nitashusha nyavu zangu. Tena kwa sababu kulingana na

ufahamu wangu hatutapata chochote



Njooi wenzangu, Andrea, Yakoba na Yohana! Tutaweka chombo tena na tutajaribu mara nyingine tena!



Haiwezekani! Wengi namna hii? Nyavu zitakatika!

Nyie kule jamani, njooi huku mtusaidie!



Nyie kule jamani, njooi huku mtusaidie!



Na vuta chombo ufukweni ama sivyo...



Haya Ni maajabu! Sijaona samaki wengi namna hii hata siku moja!



Oh! Yesu niseme nini? Nisaidie kukuamini zaidi!

Nimeanza kujifunza kutofanya kama tulivyo zoea bali kama ulivyo elekeza.

Usiogope, Simoni Petro, kuanzia sasa hutavua samaki! Bali watu!



Ndiyo! Rafiki zangu nifuateni! Nitawafanya muwe wawuvi wa watu!

Basi wakaacha vyombo na nyavu zao wakamfuta Yesu!....



Yesu alitembea Galilaya yote, akihubiri habari njema na kuponya wagonjwa na makundi yalimfuata



Wakati wangu umefika! Ufalme wa mbingu u karibu! Unapiga hodi kwenye mlango! Badilisheni maisha yenu na kumgeukia Mungu na mumtumikie.

Natamani ingekuwa kweli. Tumechoshwa na wafalme na watawala mapinduzi na mabadiliko ya serikali.

Katika vizazi vyote mifumo ya utawala iliyotoka kwa watu ni ya kusikitisha tu. Tunahitaji hakika huruma ya Mungu.

Manabii wote waliandika kuhusu Masiha anayekuja na ishara gani tutamtambua! Vipofu wataona na vilema kutembea!

Watu wenye magonjwa ya kuambukiza ni lazima waishi peke yao. Wanamngojea Yesu kwenye mlango wa mji.

Njoooni nyote ambao mmechoka na kulemewa na nitawapa pumziko! Jifunzeni kutoka kwangu, mimi ni mpole na mwenye roho ya unyenyekevu.

Ninaweza kutembea tena! Asifiwe Mungu!

Nasikia kengele za mkoma! Tusogee pembeni.

Yesu amegusa macho yangul! Sasa naona



Kaa mbali na sisi!
Usije karibu! Wewe
ni mchafu!



usimguse!
Anaambukiza!



Yesu kama
unataka
unaweza
kuniponya!



Kwa sababu
unaniamini... basi
pokea uponyaji



Nahisi
mabadiliko
ndani yangu!



Sasa nenda
ukajionyeshe kwa
Makuhani kulingana
na sheria ya Musa.

Kwa sababu hata wewe una haki
kama wengine wote na kupata
sehemu kwenye jamii yako.



Kwenye mpaka karibu na Kapernaumu, kulikuwa na ofisi ya kodi.....



Mathayo, je unaota juu ya faida yako?

Nawaza juu ya huyu Yesu ambaye kila mtu anamzungumzia... naona kuvutiwa na huyu Nabii!

Usifanye mimi nicheke! Wewe, afisa wa forodha. Anayewafanyia kazi Warumi, ambao ni adui zetu!



Wewe mtu unayependa maisha? unayependa starehe na wanawake? Sidhani kama atakupenda!

Labda unasema kweli, lakini ndiye huyo anakuja!

Shalom, Mathayo! je ungependa kuwa mwanafunzi wangu?

Ninie? Nanie? Mimi?



Mara ghafla...

Yesu ninaahidi nitakufuata wewe!

Rafiki zangu nina habari njema

Ninawaacha na kumfuata Yesu! Mnashangaa? Lakini hakika anataka mimi nimfuata yeye!



Na kusherehekea kuondoka ninaandaa karamu kubwa, na Yesu naye atakuwepo, nyote mnakaribishwa.



Jioni siku moja baadaye....



Yesu, angalia baadhi ya hawa Mafansayo ni wapelelezi, wanasema kwamba mambo unayoyafanya ni aibu!

Hakikal!



Nabii gani huyu!

Hebu mwangalie anafanya sherehe na hawa watoza ushuru wanaokula rushwa na watu waovu sugu wa mjini!

Hamwelewi kitu. Siyo wenye afya wanaohitaji Daktari, lakini walio wagonjwa! Afadhali mngewaza juu ya yale yaliyoandikwa; Mungu anasema...



Napenda msamaha, sio dhahibu! 'nampenda mtu mwenye huruma na msamaha!

Siku moja wakazi wa Kapernaumu walikusanyika kwenye nyumba ya Simoni, yule mvuvi mahali Yesu alipo, kila mtu anataka kumsikia.....



Twende na tujue huyu Yesu ni nani, tutamfuata kwa siri.

lakini itabidi tuharakishe, kama tunataka tupate nafasi ndani ya nyumba.



Si unaona? mlango umezingirwa na watu, na hatuwezi kuingia!

Tafadhali tafuteni mbinu! ingawa inaonekana haitawezekana, ni lazima nimwone Yesu! Yeye pekee anaweza kuniponya!



Najua tutapanda kwenye paa

Yohana, nenda mkalete kambal



Kwenye paa la nyumba kulikuwa na vigae vilivyotengenezwa na udongo wa mfinyanzi. Kulikuwa na uwezekano wa kung'oa vigae hivyo.



Tafadhali acheni nafasi kwa ajili yake



Lo! Watu hawa wana ujasiri kweli!

Ni yule mwenye ugonjwa wa kupooza, maskini huyu... kwa hakika hauwezi kutibika, kila mtu anajua.



Rafiki yangu... Nimeona imani yako, niamini, dhambi zako zimesamehewa!





Siku chache baadaye, kule Magdala, kijiji kisicho mbali na Kapernaumu, mbele ya nyumba ya tajiri mmoja aitwaye Simoni....



Simoni huyu Yesu anakuja hapa. Tungependa utusaidie... Tusikilize kwa makini.

Sisi tunafanya uchunguzi juu yake. Unapomkaribisha kwa ajili ya chakula cha jioni, tungependa kuchunguza zaidi na kwa karibu zaidi.

Hiyo ni sawa tu kwangu. Niooni na mpumzike na uchovu wa safari

Wakati Yesu anawasili kijiji kizima kimamngojea yeye.



Yesu wa Nazareto, karibu kwenye kijiji chetu. Sifa zako zimetanhulia mbele yako.

Huyo anakuja... Yesu mwenye kujulikana sana. Yeye ambaye hamdharau mtu. Hata wanawake wa aina yangu! Nasikia kuvutiwa kwake sana. Natamani nizungumze naye faraghani.

Nimewakaribisha watu wote wakubwa hapa kwa chakula. Tafadhali naomba tu uturuhusu kuja kwako pia.

Nakubali mwaliko wako.



Jioni ya leo atakuwa na mafarisayo... Nitajiandaa, hii itakuwa siku ya pekee kwangu.





Yule pale katikati ya wageni, moyo wangu wapiga kweli kweli... Basi nafasi yangu ni sasa au sitapata tena fursa... Nitaenda nijitupe kwenye miguu yake... na nianze kumbusu. Sijali watu watafikiria nini juu yangu! Lakini kitu kimoja ambacho nina hakika nacho! Yesu hatanifukuza kutoka kwake.



Huyu kahaba ni jasiri kweli! Yuko hapa na analia na kupangusa miguu yake kwa nywele zake?

Kama Yesu kweli ni nabii, angejua huyu mwanamke ni wa aina gani.



Ndiyo, na angempiga kibao cha usoni!

Lakini badala yake anamruhusu amguse.

Simoni nina kitu cha kukuambia



Nitashukuru niambie!



Nitakupa mithali...

Mkopeshaji mmoja alifuta madeni ya wakopaji wawili, ambao hawakuweza kumlipa. Mmoja alidaiwa mia tano na mwingine hamsini tu.

Ni yupi atayempenda zaidi?

Swali hilo lina maana yenye kina zaidi. Lakini kwa kawaida yule atayempenda zaidi ni yule aliyesamehewa deni kubwa.



Ni sawa kabisa! Ni jambo kama hili linafanyika hapa. Hujanipa maji ya kuosha miguu yangu....

Kama ilivyo desturi... hata hukunipa busu la karibu, ambalo wanapewa wageni... lakini huyu mwanamke ameosha miguu yangu na machozi na hajaacha kunibusu.....

Dhambi zake nyingi zimesamehewa... ndiyo maana ana upendo mkubwa.



Lakini yeye aliyesamehewa kidogo, ana upendo kidogo.

Binti yangu, unaweza kwenda na amani, dhambi zako zimesamehewa.

Hivi anajifikiria yeye ni nani! Anawezaje kuthubutu kusamehe dhambi badala ya Mungu!



Kuanzia siku ile na kuendelea Mariamu wa magdala, ambaye alitwa Magdalena, alimfuata Yesu pamoja na wanawake wengine.



Wakisafiri kupitia Galilaya, Yesu na wafuasi wake wanaingia kijiji cha Naini.



Inasikitisha! msafara wa mazishi ukielekea makaburini.

Unaweza kuniambia ni nani amefariki?

Mvulana... mtoto pekee wa mjane masikini. Mwanamke huyu amefadhaika mno!



Mwanamke, usilie!.....

Na nyinyi wabebaji simamenil!

....?



Tazama! Mvulana anaamka!

Sijaona jambo kama kilil!

Niko wapi?



Kijana amka!



Mwanamke, nakurudishia mwanao.

Mwanangu! Mungu asifiwe, anayetoa nguvu za namna hii!



Mtu huyu wa namna gani?

Yesu wa Nazareti, mji ulio jirani...

Nabii mpya ametokea kwetu... Mungu hasahau watu wake.

Ni muujiza hakika! Yesu ana nguvu zaidi kuliko mauti!

Kwenye ufuko wa ziwa Genesareti. Yesu alikutana na umati wa watu, ambao walipenda kumsikiliza... siku moja aliwapeleka sehemu ya mbali na kuzungumza nao hadi jioni.



Yesi saa zimepita sana na hakuna kijiji cha karibu waruhusu watu waende zao... waende wakanunue chakula.



Filipo ni lazima tuwapatie chakula.

Ni sehemu gani tunaweza kununua kiasi hicho cha chakula.

Yesu anataka kuwapa chakula watu wote hawa? Itagharimu zaidi ya dinari mia.



Kila mtu angepaswa kuleta chakula kama huyu mtoto, ambaye ana mikate mitano na samaki wawili!

Mwite huyu kijana na tuanze kugawanya chakula.

...Lakini kidogo namna hii kwa watu wote hawa?



Waambie watu wakae chini kwenye majani ili wale



Umebarikiwa ewe Mungu, kwa kuiwezesha nchi kuzalisha chakula.

Nenda ukagawanye mkate na samaki kwa wote.



Mlo huu ulikuwa mzuri. Ona ninacho chakula kilichobaki

Vema sana, ni karamu nzuri



kuleni vyote na mfurahiel!

Baada ya kila mtu kula na kutosheka.....



Kusanyeni mabaki, msipoteze kitu chochote.



Vikapu, kumi na moja, kumi na mbili, iliyojaa mikate.

Wakati huo wengine wanajadiliana juu ya mambo



Ni makuu sana mambo ambayo Yesu ameyafanya! Chakula cha kutosha wengi ambacho kilikuwa ni kidogo sana mwanzoni!



Hii inanikumbusha juu ya siku za Nabii Eliya.

Ndio, kitabu chetu kitakatifu kinaeleza kwamba siku moja alilisha watu karibu mia moja kwa mikate miwili na kupata mabaki kama tulivyopata hivi leo. Je

inawezekana Yesu akawa ndiye nabii mpya?

Lakini Yesu alitambua ya kwamba waliazimia kumfanya mfalme kwa nguvu...



Hakika ni lazima awe yule Masiha, tunayemtarajia

Peleka habari kwa kila mtu. Tunataka Yesu awe mfalme.

Tukusanyike karibu na mfalme wetu.

Tunaunda jeshi, Yeye awe kiongozi wetu tuwaondoe warumi.

Ni lazima nitoroke wamechanganyikiwa, wameelewa kinyume ujembe wangu... wanaota juu ya

Masiha mpiganaji... usiku utakopowadia nitaenda milimani!



Muda baadaye, Yesu aliongoza wanafunzi upande wa kaskazini kwenye eneo la Sazarja (siku hizi panaitwa milima ya Golani) Karibu na milima Hermoni.





Tuko mbali na umati sasa... hapo tumaweza kupumzika na kutafakari. Nataka kuwauliza swali hili, wanasema mimi ni nani?

Wao wananidhani mimi ni nani?



Oh, kuna maoni tofauti... Mfalme Herode anahisi kwa hofu kwamba wewe ni Yohana mbatizaji ambaye alimkata kichwa na sasa amefufuka kutoka katika wafu.



Wengi wanafikiri wewe ni nabii Eliya ambaye aliwatokea kwa njia isiyoeleweka na ambaye atarudi siku za baadaye.

Wengi wanasema ni nabii mpya, uliyepewa kipawa na Mungu cha nguvu nyingi.



Lakini nyinyi mnasema mimi ni nani?

Kwetu wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliyehai.

Simoni, haya hukufunuliwa na mwanadamu, lakini na Baba yangu aliyehai mbinguni!

Mungu atawafunulia haya watu wote watakaomwamini



Baada ya watu kula chakula pembeni mwa ziwa nilihubiri katika sinagogi pale Kapernaumu... watu wengi hawajakubali mafundisho yangu, na wameniacha. Je mngpenda Kuniacha pia?

Bwana tutaenda kwa nani? Tu-naamini kwamba wewe ndiwe mtakatifu wa Mungu! Unalo neho lenya uzima wa milele!

Wanafunzi wapendwa, si mimi niliyewachagua, nyinyi kumi na wawili?

Lakini, mmoja wenu ni wa shetani!



Yesu alimaanisha Yuda ambaye atamsaliti.



Mwishowe Yesu ameamua kwenda Yerusalemu

Kitu kitatokea atakapowasili kule katikaati ya sherehe... watu

wanaweza kuanza machafuko na kujaribu kumfanya mfalme kwa nguvu!


Na sisi pia tutapaata sehemu kwenye uongozi!



Kaka yangu Yohana na mimi Yakobo ndio wanafunzi wa kwanza wa Yesu. Hivyo basi sisi tutakuwa wa maana


Nini? Hamuwezi kuwa juu yetu! Kuna wengine ambao wana uwezo wa hekima kama nyinyi!

Mama mwombe Yesu atupe upendeleo.



Mwalimu, vijana wangu wawili ndio wanafunzi wako wa kwanza waruhusu waje wakae upande wako wa kulia na kushoto kwenye ufalme wako.

Hamjui ni kitu gani mnachoomba... Je mko tayari kunywa kikombe ambacho mimi nitakinywea?



Tutafanya lolote life.

Rafiki zangu mna mawazo yasiyo sahihi...
Tunaenda Yerusalemu, lakini siyo kwa ajili
ya kuwa viongozi wa siasa.


Ni lazima niende kule
na kutendewa maovu
mengi na lazima niuliwe...
lakini siku ya tatu
nitainuliwa na kuishi!



haya hayatafanyika
kwako! Haiwezekani,
tutakuja na
kukutetea wewe!

Rudi nyuma, shetani!
Unajaribu kunizuia mimi
kukamilisha kusudi langu!


Yesu nakwambia
usiwe dhai fu sasa



mnataka kwa gharama
yoyote ile mpate masiha
mwenye kupigana vita. Hivyo
inanikumbusha majaribu
ya ibilisi aliyonjaribu
kule jangwani.




'Una njaa' alinong'oneza. 'Kama wewe ni mwana wa Mungu yaambia haya mawe yawe mkate'... Nilikataa majaribu yake mimi niwe masiha Kristo ambaye hakubali kusumbuliwa na njaa... Mwanadamu haishi kwa mkate pekee, lakini kwa kila neno litokalo kwa Mungu!



Nilikataa jaribu lake al kuwa Masiha, Kristo anayewavutia watu kwa njia ya Ishara za misisimko!

Wakati mwingine nilikuwa kwenye kilele cha juu cha hekalu. 'Jitupe chini' ibilisi alinong'ona, hakuna kibaya chochote kitakachokutokea kama wewe ni mwana wa Mungu 'atakulinda na watu watakutukuza'



Baada ya hapo nilisimama kwenye kilele kirefu sana cha mlima... 'Angalia falme zote za ulimwengu na ufahari wao wote, 'Ibilisi alininong'oneza tena. Hizi zote nitakupatia kama utanipigia magoti na kuniabudu... Nikamjibu ondoka kwangu wewe shetani!

Imeandikwa mwabudu Bwana Mungu wako na umtumikie yeye peke yaka'


Rafiki zangu msianguke kwenye majaribu kama haya. Mimi ni mtumishi wa Mungu ambaye Nabii Isaya alinatangaza: Nitatoa maisha yangu kwa ajili ya watu wangu!

Ni hotuba ya kuvunja moyo tu! Ninaanza kupoteza muda wangu na nafasi yangu kwa huyu Yesu laiti ningetambua haya tangia mwanzo!

Nimechanganyikiwa. Sielewi hata kidogo...

Rafiki zangu, tengenezeni kambi chini ya mlima huu.

Na nyinyi, Petro, Yakobo na Yohana, nifuateni! Tusalala usiku huu pamoja mlimani.





Saa sita za usiku, Mwangi wa kupofusha uliwaamsha Petro, Yohana na Yakobo. Yesu alionekana mwenye nuru ya ajabu kwao na alikuwa anazumgumza na Musa na Eliya.



Baada ya tukio hilo kwisha, walimwona Yesu kama zamani.



Asubuhi kulipopambazuka, wote wanne walifunga mizigo yao na kushuka chini kutoka mlimani.

Sina maneno ya kuelezea matukio ya jana usiku.. imekuwa dhahiri kwangu kwamba

Yesu ni mkuu sana kuliko Musa na Eliya!



Nami milioniya vivyo hivyo, Yohana, nakwambia Yesu ndiye Masiha Kriso, hakika ni mwana wa Mungu aliye hai.

Rafiki zangu nawaagiza kwamba msimweleze mtu yeyote yale mliyoyaona... Mpaka mwana wa Adamu atakapofufuliwa kutoka wafu.



Kweli kabisa wao wameandaa tu kuja kwake... Yeye ni sehemu ya utukufu wa Mungu mwenyewe!

Nilisikia sauti kutoka Mbinguni ikisema 'Yesu ni Mwanangu ambaye nampenda..Mfuateni, msikilizeni!'



Petro nilikusikia ukisema, 'Ni vyema kwa sisi kuwa hapo. Kama ukipenda nitatengeneza mabanda matatu; moja lako, moja la Musa na moja la Eliya.'



Sielewi kikamilifu. Lakini tunaahidi tutakaa kimya.



Yakobo, Yohana na Mimi Petro tunaamini Mungu yupo pamoja nasi.



Njooi, rafiki Twendeni Yerusalemu!



Yesu ameamua kwenda Yerusalemu kwenye sikukuu ya Pasaka...pamoja na wanafunzi wake, Anafika kwenye mlima wa Mizeituni.

Hapa wanakutana na mahujaji kutoka Galilaya ambao pia wanaenda Yerusalemu...



Tazama! Yesu wa Nazareti yulee!

Nabii mashuhuri kutoka jimbo letu la Galilaya!

Ni lazima Tufanye maandamano wakati Yesu anaingia mjini! Watu wa

Galilaya, hebu tukusanyike na kumzunguka... Tumshangilie Yeye

kama Masiha! 'Hilo litakuwa jambo la kusisimua'!

Yesu, tafadhari walao kwa mara moja kubali ombi hili!

Nakubali

Nendeni kwenye kijiji kile ambako mtamkuta mwanapunda aliyefungwa Mfungueni na mleteni hapa....Nami nitampanda





Nani amewaambia mufungue huyo punda?

Yesu wa Nazareti yule nabii mashuhuri, anamhitaji tutamrudisha kwako.

Kama ni hivyo mnaweza kumchukua.



Na tukate matawi ya mizeituni kwa ajili ya maandamano.

Haya gaweni matawi haya!

Tutakapoingia Yerusalemu, tandazeni nguo zenu kwenye njia kama Ishara ya heshima. Na nyinyi watoto, tafuteni maua!



Na aishi Yesu wa Nazareti!

Masiha mwana wa Daudi!

Hosannah!



Ni nani mnayemshangilia?

Yesu wa Nazareti, Nabii mpya!



Hii maana yake nini?

mm... Warumi watakapata taarifa ya jambo hili majeshi yao yanaweza kuchukua hatua...

Maandamano yamewasili karibu na eneo la Hekalu...Waombaji, wagonjwa na wasiojiweza walimfuata..



Sasa watoto wanaanza kumshangilia Yesu.

Tokeni hapo nyinyi watu wachafu! Hamjatakaswa na hamruhusiwi kuingia Hekaluni.


Usijali kama mimi sijiwezi; Yesu ataniponya!



Udumu Yesu wa Nazareti!



Nyamazeni, hili ni hekalu Takatifu.





Tokeni kila mtu!

Nyinyi pia! Watu waovu mnafanya biashara kwenye

Hekalu na mnakiuka heshima ya maandiko matakatifu, 'Nyumba yangu itaitwa nyumba ya maombi kwa watu wote, 'asema Mungu lakini nyinyi mmeigeuza kuwa...



Pango la wanyang'anyi!



Vizuri sana mwishowe kuna nabii mwenye ujasiri, ni aibu kabisa, hii biashara yote kwenye hekaku la Mungu!



Na nani anapata faida? Kuhani mkuu na mafarisayo wanaouza sehemu za kufanyia biashara kwa wenye kutoa ada kubwa..



Ilikuwa ni mithali hakika. Yesu alizungumzia juu ya mwili wake. Hekalu jipya la Mungu.. likiharibiwa, atafufuka tena kutoka wafu baada ya siku tatu. Baada ya kufufuka kwake wanafunzi wake walitambua maana yake.

Muda mfupi baadaye, Mafarisayo ambao walikuwa maadui wa Yesu, walikusanyika pamoja chini ya uongozi wa kuhani Mkuu Kayafa.



Kusudi la Yesu halikufanikiwa, mimi Yuda niliweka tumaini langu la mbele kwenye kufanikiwa kwake nilitumaini yeye kama Masiha angeongoza harakati za ukombozi... Badala yake amesalimu amni... Nimedanganyika. Nisipojihadhari nitapoteza kila kitu.

Njia moja ya kufanikiwa sasa.....

Ni kuwaendea adui zake na kuwasaidia ili wamkamate.

Ninaamini viongozi wetu wasema kweli! Yesu anahatarisha usalama wa taifu letu!

Nimeamua la kufanya!



Siku chache baadaye, usiku..



Ni mimi Yuda.



Vizuri Yuda umetimiza ahadi yako



Nimeamua kumkabidhi kwenu

Yuda unafanyia taifa letu fadhila kubwa...tunatoa shukrani nyingi kwako

Basi tumekubaliana! vipande thelathini vya fedha! Huo ndio ujira ambao...tuko tayari kukulipa kwa kumkabidhi Yesu mikononi mwetu.



Fedha ndizo hizi sasa tungoje wakati unaofaa




Uwe mwangalifu isiwe hadharani maana makundi yanaweza kumtetea na hivyo kufanya kukamatwa kwake kushindikane.

Ikiwezekana iwe usiku....huo ndio wakati wetu muafaka!



Kwa majuma kadhaa Yesu na wanafunzi walikuwa wamejificha, wakati watumishi wa Kuhani Mkuu walikuwa wanamtafuta.....



Rafiki zangu, leo Pasaka inasherehekewa. Petro na Yohana, nendeni kufanya maandalizi ili tule pasaka.

Ndiyo Bwana, lakini wapi na nani?



Nimeagiza chumba kikubwa Yerusalem. Ni lazima mwende na kupatafuta.



Mnapoingia mjini, mtakutana na mtu amebeba mtungi wa maji. Mfuateni mpaka kwenye nyumba anayoingia. Basi hiyo ndiyo nyumba yenyewe.

Aha, Yesu haniamini mimi tena...lakini mimi kama Mweka Hazina ninayo haki ya kuandaa pasaka... na ndivyo nitajua mahali wanapokutana!



Na wakati huo nitakuwa nimewapasha habari watawala waje kumkamata

Masaa machache baadaye.....

Wanawake wanaobeba mitungi ya maji, hilo ni tukio la kawaida.

Lakini pale namuona mwanamume amebeba mtungi, hilo si jambo la kawaida! Je inawezekana ndiye yule mtu?

Ni lazima awe! Basi tumfuateli!





na hiki ndicho chumba kikubwa kilichoandaliwa kulingana na maaqizo ya Yesu. Kama mnavyooha, kila kitu kumepangwa barabara.



Jioni siku ile..



Rafiki zangu nimetamani sana kula pasaka hii pamoja nanyi kabla ya kuteswa na kutoa maisha yangu, ili wengi waokolewe.



Walikusanyika kwenye meza, lakini kulitokea kutokuelewana



Niachie nafasi hii mimi. Mimi nina haki ya kuwa karibu na Yesu.


Hapana nipo hapa na nitakaa hapa hapa! sisi sote hatuko kwenye kundi moja?

Ndiyo, hivyo ni kwejil Hakuna upendeleo! Hakuna nafasi maalumu kwa mtu!

Rafiki zangu ngojeni kidogo, kabla ya kuchukua nafasi zenu...



Mnajua kuwa wafalme wa mataifa huwanyanyasa raia walio chini yao, wanawatawala watu wao kwa upanga na mabavu, lakini ninyi hamko namna hiyo....



Badala yake, wajibu wenu ni kutumikiana ninyi kwa ninyi.

Baada ya hayo.....



Angalieni jambo analofanya

Sielewi kitu gani anataka kufanya! Inaelekea anajiandaa kufanya usafi.





Nini? Lakini... unataka ku...



Kuosha miguu yangu?

Bwana, miguu yangu Hapana hutaniosha kamwe miguu yangu?



Huelewi sasa kitu ninachokifanya, lakini baadaye utaelewa... Nisipokuosha huna ushirika na mimi... na huwezi kuwa rafiki yangu.



Oh, basi nafuta yote niliyoyasema! siyo miguu tu lakini na kichwa na mikono pia unioshe!



mtu ambaye ameoga anahitaji tu kuosha miguu yake. Ninyi ni safi sasa...




Ingawa si nyote...

Jambo analofanya mwalimu, ni jambo la kujidhalilisha! hiyo ni kazi ya mtumwa!

Alisema maneno haya Yesu aliwaza juu ya Yuda Iskariote...

Wakati Yesu alipomaliza alisema...



Mmelewa kitendo nilichowafanyia? Mnaniita mwalimu na Bwana, na hivyo ni kweli. Maana ndivyo nilivyo. Sasa kama mimi, Bwana wenu, nimejifanya mtumishi wenu, nimewapeni mfano kwa hiyo tendeaneni ninyi kwa ninyi namna hiyo.

Walipoanza kula Yesu na wanafunzi wake walikula saladi chungu, kumbukumbu siku za mateso ambazo mababu walipitia kule Misri kabla ya siku zile za kutoka.



Rafiki zangu nina jambo la huzuni la kuwaambia. Mmoja wenu atanisaliti mimi.

Ndiyo, nasisitiza neno hilo ni mmoja wenu, anayekula kwenye meza hii hii....

Anasemaje? Jambo hilo linawezekana kweli? litakuwa jambo baya mno!

Ni nani kaati yetu anayeweza kufanya hayo?



Au mimi?

Natumaini husemi kwamba ni mimi?



Simeoni Petro anamngong'oneza Yohana na anamwambia; Mwulize anamaanisha ni nani... tunaweza kujaribu kuzuia jambo hilo lisitokee.





Yesu, niambie ni nani?

Ni yule nitakayempatia kipande hiki cha mkate...



ambacho nimechovya katika bakuli



Kile unachotaka kufanya kifanye haraka.



Je umeona hayo? Si heshima kubwa hiyo!

Ndiyo hiyo ni ishara ya heshima kwa Yuda, sawa?



Baada ya Yuda kupokea kupande cha mkate aliamka na kutoka nje



Na ilikuwa usiku




Yuda anaenda wapi?

Sijui labda Yesu amemtuma aende kununua kitu fulani...

au kuwapatia maskini vitu kama tunavyofanya kila mara wakati wa Pasaka.

Baada ya Yuda kuondoka, Yesu alitoa ishara ya kuanza kula. Akatoa shukrani..



Sifa ni kwako, Mungu wetu, kwa kutupatia chakula hiki!

Alimega mkate na kuwagawia...



Lakini aliendelea kusema.....



Twaeni na mle: huu ni mwili wangu, uliovunjwa kwa ajili yenu.



Baada ya kula mkate Yesu alichukua kikombe na kushukuru



Lakini aliendelea.....




Halafu Yesu na wanafunzi wanamaliza kula na kuimba nyimbo za pasaka.



Na baadaye waliondoka Yerusalemu...



Yesu na wanafunzi walitelemka mpaka kwenye bonde la Kidroni....



Baada ya kuvuka mto Kidroni, walianza kupanda Mlima mzeituni.

Rafiki zangu nawaonya usiku huu wa leo mtanionea aibu na nyote mtaniacha...



Wengine wanaweza kuona aibu, mimi siwezi! Hata kama ikibidi nife, sitakukana kamwe!



Petro usiku huu kabla ya jogoo kuwika mara mbili wewe mwenyewe utanikana mara tatu!



Wakaenda bustani iitwayo Gethsemane.....

Kaeni hapa... Nitaenda mbele pamoja na Petro, Yakobo na Yohana.



Yesu aliwachukua wanafunzi watatu pamoja naye....



Yesu alirudi kwa wanafunzi wake apate faraja, lakini...





Wakati huo kwenye mlango wa bustani...



Baada ya mshituko wa kwanza, wanafunzi wa Yesu wakajizatiti ili kujitetea.....



Na hamtasahau hayo siku zote za maisha yenu AUGH! AUGH!



Mbona mmekuja kwa siri, usiku ili mtukamate! Nitawafunzeni adabu!



Petro rudisha upanga wako alani!

Maana wote wanaotumia upanga, watakufa kwa upanga!

Je mimi naongoza, maasi hata mnanijia kwa mapanga na marungu kunikamata?

Kila siku nalikuwa kwenye hekalu nikifundisha... hamkunikamata pale... Lakini huu ndiyo wakati wenu... Wakati wa giza linatawala.

Yesu aliwaruhusu wamkamate... baada ya kuona haya, wanafunzi wote walimwacha na kukimbia.



Kikosi cha askari walimchukua Yesu kutoka mlima wa Mizeituni hadi Yerusalemu...



Wamempeleka kwenye nyumba ya Kuhani Mkuu.





Simwamini yule mgeni aliyeingia

...alikuwa pamoja naye Yesu?

?



Unasema juu ya nani? Yesu wa Nazareti? mimi simfahamu!



Nilikuwa napita tu ... na baridi ni kali sana usiku wa leo, basi nikaja ili niote moto

Hakika? lakini matendo yako yananita shaka, wewe ni mmoja wa wanafunzi wake.



Nisikilize nakwambia...

Kwamba simjui mtu yule!

Wakati huo kwenye makao rasmi...



Yesu anapelekwa kwa Kuhani Mkuu. Ambaye ameitisha mkutano wa Wakuu wa Makuhani na wazee na wlimu wa sheria...



Nimewaite mje mchunguze kesi ya Yesu wa Nazareti maana maslahi nyeti sana ya taifa letu yako mashakani!

Vitimbwi vyake vya kusisimua vinaathiri utulivu katika jamii. kauli zake za kimapinduzi kinyume cha hekalu na dini yetu, yamenifanya niamuru akamatwe...



Na aletwe mbele mbele ya mahakama yetu ili tuweze kumshitaki kwa mujibu wa sheria zetu. Leteni mashahidi!



Nilimsikia akisema "Mnaweza kuvunja hekalu hili na baada ya siku tatu nitakuwa nimelijenga upya!

Hapana, hakusema hivyo! Bali, "Nitalivunja hili hekalu lililojengwa na mwandamu na nitalijenga lingine ambalo halikujengwa na mwanadamu"



Ni vigumu kuamini kwamba alijaribu hata

kusema kinyume cha utukufu wa Mungu na hekalu.



Nitaandika mashahidi hawakubaliani. Yesu hajajibu lolote...Mkutano umegawanyika na kuchanganyika na kuchanganyikiwa.





Tuache haya mazungumzo kuhusu hekalu, kwa sababu mshitakiwa hajibu kitu.... Na tuendeleee.....

Yesu tuambie wazi je wewe ndiye Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai?



Ndiyo, mimi ndiye na

mtamwona Mwana wa Adamu amekaa mkono wa kuume wa Mungu mwenyezi na akija mwinguni kutoka mbinguni

Amesema kufuru!

Kwa nini tunahitaji mashahidi zaidi? Tzama, nyote mmesikia kufuru!



Anastahili kufa!




Je mnaonaje?

Na huyu Yesu anajifanya mwana wa Adamu ambaye nabii Danieli alimzungumzia kwenye ndoto. Mtu atakayepelikwa mbele za Mungu ambaye atapewa nguvu na mamlaka juu ya mataifa yote.

Ni kufuru iliyojaa kiburi hasa!

Ninaandika majaji wote wamegadhabishwa baada ya kusikia kufuru hii na Kuhani Mkuu kararua mavazi yake kuonyesha namna alivyochukizwa.





Basi kesi imeamuliwa lakini, kwa kila hukumu ya kifo...

ni lazima kibali cha Gavana wa Kirumi kipatikane.

Ndiyo hivyo ni kweli. Ni yeye tu anayeweza kupitisha hukumu ya kifo na kumfanya mtu

auliwe. Tumpeleke Yesu kwa Pilato ambaye yuko Yerusalemu kusimamia sherehe ya pasaka.

Kolo_m kooh

Wakati huo uani kwenye watu waliozunguka moto...



Siwezi kuona ajabu kama wewe nawe ulikuwa pamoja na Yesu!

Ndiyo, wewe ni Mgalilaya, matamshi yako yanaonyesha wazi!

Petro alianza kulaani na kuwaapia: mimi simjui huyo!



Lakini, Oh....



Kolo_m kooh
Kolo_m kooh



Sasa nakumbuka maneno ya Yesu: « Kabla ya jogoo kuwika mara mbili utanikana mimi mara tatu. » Ooh mimi ni mwoga.... Mwoga kweli wa kupindukia!

Yuda alisikia kwamba Baraza limemhukumu Yesu.



Akijawa na majuto alikwenda haraka hwenye baraza na kurudisha vipande vile thelathini vya fedha.....



Sitaki fedha zenu!



Hilo ni shauri lako, sisi halituhusu!



Akiwa amekata tamaa, Yda aliondoka kwenda kujinyonga.



Asubuhi niliyofuata Yesu alipelekwa Pilato...



Na wasaidizi wa baraza.....





Basi wewe ni mfalme?

Ndiyo mimi ni mfalme

Na kwa kweli kwa kusudi hili mimi nilizaliwa na kuja ulimwenguni huku ili kushuhudia juu ya kweli. Yeyote aliye upande wa kweli ananiskiliza mimi.

Kweli? Ukweli ni nini?



Ni jambo dhahiri kwamba simshughulikii mtu ambaye eti ni mchochezi wa hatari, msumbufu mwenye hatari, yamkini ni mtu tu wa falsafa fulani... au mkereketwa wa aina yake..... lakini hamasa kubwa ya Mafarisayo kinyume na makini... kwa sababu sitaki kuburuzwa na watu katika kutoa uamuzi



Mchukueni mshitakiwa kwenye chumba cha walinzi!



Haya, huyu ndiye anayejizania kuwa mfalme

Mfalme?



Mtukufu, njoo hapa! tunataka kujiburudisha...



Kaa hapa chini

Oh hili ni vazi zuri sana la kifalme!

Hili linakufaa sana wewe mtukufu!



Lakini taji bado linakosekana!



Na hii ndiyo fimbo ya utawala.

Na sasa wenzangu, sisi sote na twende kwake na kusema "Salaam Mfalme wa Wayahudi"



Haya sas unalo taji!

Wakati huo kwa Pilato.....



"Salaam mfalme wa Wayahudi"



Makundi ya watu yanaingia mjini!







Nyamazeni nitawaleta wafungwa wawili mbele. Nanyi mfawaangalia na kufanya uchaguzi bora zaidi.



Walinzil! mleteni Yesu na Baraba hapa!



Mwangalieni mtu huyu!

Hapana siyo Yesu, tunamtaka Baraba!

Baraba! Tunamtaka Baraba yeye mwachie huru!

Msulubishe! Msulubishe Yesu! Anastahili kufa!

Ndiyo mwiteni Baraba! Huko ndiko kutetea maslahi rahisi ya Taifa!

Yesu ni mchochezi anawadanganya watu! Anastahili kuuawa!



Baraba!

Baraba!

Hamuoni aibu kudai Yesu wa Nazareti auawe?

Nabii ambaye anaponya wagonjwa, vipofu na wenye kupooza...na kuwapatia maskini tumaini na wote wanaogandamizwa na wote wasio na tumaini?



Oh angalieni! udhalimu mkubwa huo! wamempiga Yesu!

Na tulidhani ndiye Masiha tunayemtarajia!

Mnataka kunilazimisha kumhukumu Yesu asulubiwe. Basi mchukueni na msulubisheni wenyewe! Maana mimi sioni kosa lolote!

Hatuna haki yoyote ya kumwua... Lakini kulingana na sheria zetu ni lazima afe, kwa sababu anajidai kuwa ni mwana wa Mungu.

Uwe mwangalifu Pilato! unajiingiza mwenyewe kwenye matatizo!

Yeye adai kuwa ni mfalme. Kwa hiyo anampinga Kaisari wa Roma! kama ukimwacha huru, huwezi kuwa rafiki ya Kaisari.

Tafadhali usihatarishe wadhifa wako! pakipungua au kuongozeka Myahudi mmoja, weve utaathinka vipi?

Usinga'ng'anie sana kumtetea huyu mtu asiye na makosa. Viongozi wa taifa lake wanataka afe kwa gharama yoyote... Kama ukimweka huru watalalamika kwa mfalme Tiberia juu yako...

Wakazi wa Yerusalemu, je, nimsulubishe mfalme wenu?

Hatuna mfalme isipokuwa Kaisari wa Roma.



Kwa nini awe mfalme wetu? kwa kuvaa tu hili taji la miiba na hilo vazi la dhihaka?

Masiha? Huyu..Mfalme wetu? Mwondoe mbali! Msulubisha!

Msulubishe!

Unataka kumfanya nani mjinga, Pilato?



Mnawajibika ninyi!

Nanawa mikono kuonyesha kwamba sina lawama mimi.



Hukumu yangu ni Baraba umewekwa huru Pasaka hii kutokana na matakwa ya wakazi wa Yerusalemu. Wewe Yesu wa Nazareti, utasulubishwa.



Uishi maisha marefu, Baraba!

Uishi maisha marefu Baraba!



Oh! wenyeji halisi wa Yerusalemu hawakuwepo hapa kumtetea Yesu!... waliokewepo ni mashabiki tu wasio na maana wa Baraba!



Huyu ndiye badala ya Baraba.



Anajifanya kuwa mfalme. Kwa hiyo mpatieni huduma kamili ya kifalme.

Usiwe na wasiwasi tutamshughulikia ipasavyo.



Siku ya leo watu watatu watapata adhabu ya kifo na kulingana na desturi, kila mtu aliyehukumiwa lazima apigwe mijeledi




Hiyo ni kwa mfalme wa Wayahudi... Nafikiri ametosheka

Sasa Yesu lazima abebe nguzo ya msalaba wake, akiwa na tangazo kifuani mwake, linalotangaza hukuma yake.



Na maandamano ya kuhuzunisha yanaanza kwenda.....



Tokeni njiani! Tuacheni tupitel!

ni nani yule?

Anafanana na Yesu wa Nazareti... Nabii mashuhuri!

Hapa tunamwona mtu ambaye alifanya mema; aliponya wagonjwa, na kutetea haki ya maskini na wanaogandamizwa! Oh, haki imekiukwa kabisa!

Ole wao! katika chuki yao walimkabidhi kwa Warumi.

Mafarisayo walimchukia kwa sababu alisema ukweli na kuweka wazi unafike wao!

Mmoja ameanguka chini!



Amekuwa dhaifu sana kubeba msalaba wake: amepoteza damu nyingi kwa sababu ya kupigwa mijeledi.



Hey, wewe! Nimekuamuru kubeba msalaba huu wa huyu mhukumiwa mpaka Golgota! Hiyo ni amri! Lazima utii!



Mimi ...lakini mimi si mkazi wa Yerusalemu! Mimi ni raia mwema kutoka Kirene!



Uwe na busara na ubishi ama sivyo utakuja kujuta. Warumi ni wajeuri hata hivyo hapa siyo mbali na Golgota.

Nitaku-bebea! Wewe simama!



Msaidie hana hatia Ni Yesu wa Nazareti, nabii Mkuu...



Mabinti wa Yerusalemu mbona mnanililila mimi? Ni afadhali mijililie ninyi na watoto wenu.....

Maana muda si mrefu toka sasa pigo kubwa litashuka juu ya Yerusalemu.



Tazama, hapo ndipo mahali pa adhabu ya kifo, panaitwa Golgota, yaani "fuvu la kichwa"


Kutoka mbali mwamba kweli una sura ya fuvu.

Na sehemu imechaguliwa vizuri! Kila mtu anayekuja Yerusalemu alikumbushwa gharama ya kuwapinga Warumi.



Walipofika Golgota, walimvua Yesu nguo kikatili.

Ziweke nguo zake pale, tutazigawa baadaye!









Nimeona wafungwa wengi wakifa. Lakini huyu! Hakika huyu mtu alikuwa mwana wa Mungu!



Kapeni, ujumbe kutoka kwa Pilato!



Pilato ametoa amri miguu ya washitakiwa kuvunjwa na miili yao itolewe kutoka kwenye misalaba. Wayahudi hawataki miili iachwe wakati wa Sabato. Maana hiyo italeta laana juu ya watu.

Askari anza kuvunja miguu ya wafungwa, ili wafe haraka!



Tayari ameshak ufa

Na tumpige mkuki ubavuni kuhakikisha...



Kutoka kwenye moyo wake ilimwagika damu na maji.

Wakati huo....

Yusufu wa Arimathaya...



Fanya haraka, Nikodemo, usiku umekaribia!



Yesu alikufa kama mhalifu.. na ninaamini kwamba hakika alikuwa Masiha.

Nilimwomba Pilato anipatie kibali cha kuchukua mwili wa Yesu ili nikauzike.



Siyo mbali na hapa. Nina bustani yenye pango jipya na kaburi ambalo halijatumika... Nimeamua kuuzikia mwili wa Yesu pale.




Baada tu ya kusikia kifo chake, nilichanganya marukato...na Yusufu analeta sanda na mikanda ya kumzungushia..

Na yufanye haraka, kabla ya tarumbeta haijaliala kutangaza Sabato na Pasaka... Baada ya hapo haturuhusiwi





Na mwishowe jiwe zito lilingirishwa kwenye mlango wa pango...



Asubuhi na mapema, siku iliyofuata Pasaka ya Sabato, wanawake wanaenda kwenye pango...





Yohana, Petro!
Nimetoka moja kwa
moja kwenye pango.
Lakini liko tupu!
Mwili wa Yesu
umetoweka!

Wacha
twende
tukaangalie
wenyewe



Petro
nenda
wewe
kwanza!



Yohana
unakimbia sana!
Ninashindwa
kupumua!



Yohana, tazama
hapa...



Lile sanda ambalo Yesu
alikuwa amevingirishiwa
halijaguswa, sijui ni kitu
gani kimetokea.



Mwili wa mfu huwa
hauibwi namna hii! Ama
unachukuliwa na nguo zake.

Sina la kusema!
Sijui jinsi ya
kulifafanua!



Twende zetu!
Hatuwezi kufanya
jambo lolote hapa.

Sasa naelewa!
Naamini amefufuka
kutoka wafu!

Maria Magdalena amerudi kaburini...Anashangaa na kulia...



Bibiye, mbona unatafuta mtu aliye hai katikati ya wafu?

Mbona unalia? Kuna tatizo gani?



Mtunza bustani kama umemwondoa mwili wake, niambie umemhifadhi wapi...



Maria!

Bwana Yesu?



Bwana wangu

Usijaribu kunishika



Kwa maana ninarudi kwa Baba yangu wa mbinguni, lakini nenda na uwaambie wanafunzi wangu!



Jamani nememwona Yesu, Bwana! Yeye yu hai amefufuka! Sikilizeni aliyoniambia!



Mariamu hisia zako zimekuchanganya akili!

Tumia akili na busara, jambo hilo haliwezekani!

Hizo ni ndoto! Ni mawazo tu ya wanawake!

Siku hiyo hiyo, jioni wawili kati ya wanafunzi walikuwa wanasafiri kutoka Yerusalemu kwenda Emau....



Ni jambo la kuvunja moyo sana! Nilimwamini Yesu na kufikiri ni Masiha aliyengojewa na dunia.



Na badala yake alihukumiwa kifo na kusulubishwa kama mhalifu

Ndio Cleopa, ni jambo la kuvunja moyo! Mimi nimechanganyikiwa kama wewe...

Shalom, rafiki! Mnaonekana wenye huzuni... mnajadiliana nini? Jaribuni

kunieleza labda naweza kusaidia.



Wewe hujui mambo yaliyotokea na kuitikisa Yerusalemu siku hizi? Mambo kuhusu Yesu wa Nazareti?



Tulitumaini ya kwamba, yeye ndiye yule atakayekomboa Israel...

Ndiyo maana alikuwa Kristo... Lakini yamekwisha... Ni...

Siku ya tatu tangu mambo haya yalipotokea na sasa amekufa.

Baadhi ya wanawake kundi letu wametustaajabisha ...

Walienda kwenye pango asubuhi na mapema...





Lakini hawakuukuta mwili wake... wakatuambia kwamba, eti waliona malaika ambao walisema "YU HAI!"

Wanawake ni wazushil baadhi ya rafiki zetu walienda kwenye pango na kulikuta tupu kama vile wanawake walivyosema, lakini hawakumkuta Yesu... sasa hatujui tufikiri namna gani.

Mmekuwa wajinga kiasi gani, na wazito kiasi gani wa mioyo kuamini yale ambayo Manabii waliandika!



Saa moja baadaye.....



Hebu niwafunulie yale yaliyosemwa katika maandiko yote kuhusu yeye...

Tunakusikiliza kwa makini sana.



Tumewasili Emau.... Tunakukaribisha ukae nasi.



Hakuna tatizo lolote! kaa nasi, na utaendelea na safari yako kesho.

Asante sana nakubali.



Walipokuwa mezani, alichukua mkate, akashukuru, akaumega, akawapatia....

Basi macho yao yalifunguliwa na wakamtambua.



Lakini alitoweka ghafla kati yao.

Harakisha na turudi Yerusalemu!

Ni lazima tukawaambie wanafunzil!

Yesu yu hai! Yesu yu hai!



Moyo wangu ulikuwa unawaka ndani....alipokuwa anafafanua maandiko

Hata mimi! Mwanzoni sikuelewa...lakini alifanya mambo yote kuwa dhahiri



Rafiki tusikulizeni tuna habari kuu mno!

Tusikulizeni sisi kwanza! Yesu yu hai! Amefufuka amejiyonesha kwa Simoni Petro



Sasa nisikulizeni na mimi: tulimtambua alipomega mkate.



Ghafla Yesu alisimama kati yao....

Amani na iwe kwenu rafiki zangu



Ninamwona nani? Huyu ni Yesu ama naona mzuka?

Kwa nini mu wagumu wa kuamini? Je mzuka una mwili na mifupa kama niliyonayo?



Yesu anaishi, ni furaha iliyoje! Oh, ni kweli yu hai!

Wengine wenu bado mna mashaka... je mnacho chakula?



Hiki kipande cha samaki wa kubanika.

Maandiko yanatangaza kwamba Kristo atateswa na kuuawa, lakini pia kwamba atafufuka kutoka wafu.

Nyinyi nyote ni mashahidi wa haya! Hubirini habari njema ulimwenguni kote!



Yesu aliyefufuka alionekana kwa wanafunzi siku iliyofuata Pasaka. Juma moja baadaye walikutana tena...



Tomaso yule anakuja. Bahati mbaya hukuwepo wiki ilipita, ungemwona Yesu.

Jambo la namna hii halijawahi kutokea, lakini ni kweli alikuwa kati yetu!



Nyinyi nyote mmerukwa na akili...

Hamuwezi kunihadaa mimi na porojo kama hizo!

Sikiliza Tomaso, tulikuwa tumekusanyika kwa siri. Milango yote ilikuwa imefungwa tukiwa na hofu ya...



Wayahudi..na ghafila Yesu alikuja na kusimama kati yetu! Afadhali ungekuwepo pamoja nasi.

Ninaelewa, mmeshindwa kusahau mkasa huu ndiyo maana tangu....

Kifo chake mnamwona kila mahali.



Fahamu zenu zimewachanganya akili.



Tomaso hatukuota ndoto; alituonyesha makovu ya mikono na kwa hakika tumemwona!

Lakini hamkumgusa! Ingebidi mfanye hivyo!

Hapo ndipo mngegundua kwamba mnajifurahisha na ndoto tu! Nisipoona alama za misumari mikononi mwake na kwa mkono wangu kumshika ubavuni,sitaamini! Hata!



Ghafla wanamona Yesu amesimama kati yao.

Amani iwe nanyi rafiki!

Tomaso...

Njoo hapa!



Sasa weka mikono yako hapa, angalia mikono yangu.

Na uweke mkono wako kwenye ubavu wangu!


Acha kuwa na mashaka bali uamini!



Nakuamini Bwana, na Mungu wangu!



Tomaso unaamini kwa sababu umeona, wamebarikiwa wale wasioona na lakini wanaamini tu!



Jamani, naenda kuvua samaki usiku wa leo!

Tutakuja pamoja na wewe...

Usiku ule hawakupata kitu.

Kulipokucha Yesu lisimama ufukoni.....



Je mmepata samaki?

Hapana, hatukupata kitu!

Ni usiku mbaya sana! Tumechoka sana na hatukupata kitu.






Muda mfupi baadaye, wakati walipokuwa wanavuta nyavu ndani ya chombo....







Kwenye mlima wa Mizeituni, wanafunzi walimwona Yesu akienda mbinguni na atarudi hivyo hivyo **HIVI KARIBUNI!!!**



Upendo wa Mungu Kwako Wewe

Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.

(Yohana 3:16)

Bali Mungu aonyesha pendo lake yeyemwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.

(Warumi 5:8)

Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi.

(Yohana 14:6)

Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Mwana wake, yatusafisha dhambi yote. Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu. tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote. **(1 Yohana 1:7-9)**

Bwana zangu, yanipasa nifanye nini nipate kuokoka? Wakamwambia, Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako.

(Matendo 16:30-31)

Habari njema ni kwamba: Yesu amefufuka kutoka wafu Anaishi!

Sala:

Yesu, naamini kwa moyo wangu wote kwamba ulikufa kwa dhambi zangu pia. Nakiri dhambi zote na naomba msamaha wako. Njoo uishi moyoni mwangu, kuazia sasa na kuendelea itakuwa maishani mwangu kwamba:
Si mapenzi yangu, bali mapenzi yako yatimizwe.
Nashukuru kwamba unataka kuwa mwokozi wangu.
Amina !